KIGOMA HABARI ZA MKOA
News Bulletin
Web: http://www.kigoma.go.tz

Toleo Na. 006 Habari za Kila Mwezi 31 Agosti 2024



Uwepo Shule ya Wasichana Kuondoa adha kwa Wanafunzi wa Kike Mkoani Kigoma



Mchengerwa aibana TARURA Barabara Wanazojenga Mkoani Kigoma



Afya Ngazi ya Jamii ya pokea Usafiri Kigoma



Mchengerwa atoa miezi sita kutowepo vifo vya mama wajawazito Kigoma

# Matumizi ya Shilingi trilioni 11 kwenye miradi ya Maendeleo Mkoani Kigoma yamkuna Mchengerwa.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) akikagua ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Kigoma iliyopo Wilaya ya Uvinza.*

## Dhamira ya Serikali ni Kuufungua Mkoa wa Kigoma Balozi.Dkt Nchimbi

Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi amemuelekeza Waziri wa Nishati kufuatilia na kushughulikia changamoto ya kukatika kwa Umeme mara kwa mara wilayani Kasulu na kuitafutia ufumbuzi wa haraka ili uhakikisha wananchi wanapata huduma hiyo kwa uhakika na kuruhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo.



Balozi.Dkt Nchimbi

## Maafisa Ugani Kilimo Kigoma Wachekelea Neema ya Rais Dkt Samia

- Sekta ya Kilimo kuwawezesha wakulima kufanya kilimo biashara chenye Tija.
- **Halmashauri za kumbushwa kutekeleza Maagizo ya Wizara**



## Shughuli za Uvuvi Ziwa Tanganyika Zarejeshwa



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amezindua zoezi la uvuvi katika Ziwa Tanganyika baada ya kupumzishwa kwa shughuli za uvuvi katika ziwa hilo kwa muda wa miezi mitatu.

# Waziri Mohamed Mchengerwa (Mb) aridhishwa na matumizi ya Fedha zaidi ya Shilingi Tril.11 Mkoani Kigoma.

Mhe. Mchengerwa ametoa kauli hiyo alipozungumza mara baada ya kuhitimisha ziara yake ya Siku tatu mkoani Kigoma na kusisitiza kuwa pamoja na matumizi mazuri ya fedha hizo yapo maeneo hakuridhika na utekelezaji wa miradi kutokana na kukwamishwa na wasimamizi wa miradi hiyo jambo linalochangia kwa kiasi kikubwa kukwamisha maendeleo ya wananchi

Amesema katika maeneo yote aliyobaini baadhi ya watendaji wa Serikali kutumia kinyume na utaratibu fedha zinazotolewa na Serikali, ametoa maelekezo sambamba na kuchukua hatua dhidi ya watendaji walioshiriki kukwamisha miradi ya serikali.

''Tunakwenda kukutana na watendaji wenzangu walio chini ya wizara hii ili kuandaa Taarifa kamili kwa ajili ya kuchukua hatua katika maeneo yote ambayo watendaji hawakufanya vizuri kwa sababu za kushindwa kuwajibika'' amesema Waziri

''Nasisitiza hata kama mtumishi amehitimisha muda wake wa utumishi serikalini, amehamishwa au uteuzi wake umetenguliwa tutamrejesha hapa ili aweze kujibu makosa yake iwapo tutathibitisha kuwa mtumishi huyo alishiriki kupokea rushwa, kusababisha ubadhirifu au aina yoyote ya upotevu wa fedha za serikali hatutosita kuchukua hatua''amesisitiza Mhe. Mchengerwa.

Mchengerwa ametoa wito kwa viongozi wote wa serikali kukumbuka wao ni watumishi wa wananchi, hivyo watumie nafasi zao kuwatumika watanzania. Ukiwa waziri, Mkuu wa Mkoa, mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi nk, jitahidi kuwatumikia wananchi ili uweze kuacha alama kwa unaowatumikia na Taifa kwa ujumla.

Awali waziri huyo amekagua jengo la Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya ya Uvinza na kuielekeza TAKUKURU

kufanya uchunguzi kuhusiana na ujenzi wa jengo la ofisi hiyo kutokana na waziri huyo kubaini baadhi ya kazi zilizofanyika katika ujenzi wa jengo hilo kutozingatia miongozo ya serikali na kukosa ubora.

Aidha amemuelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo



Jengo la Utawala katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Kigoma

kuhakikisha ndani ya Siku mbili kuanzia Agosti 14, 2024, jengo hilo linaunganishwa kwenye mfumo wa Umeme ili kurahisisha utendaji kazi wa watumishi wanaotumia ofisi hiyo

Akiwa katika shule ya sekondari ya Uvinza Wasichana, Mhe. Mchengerwa amemuelekeza mhandisi wa Wilaya hiyo kuhakikisha huduma ya Umeme inafika kwenye mabweni yote ya shule hiyo.

Aidha Mchengerwa amepata fursa ya kuzungumza na wanafunzi wa shule hiyo na kusisitiza kuwa Mhe. Rais anaguswa na changamoto ya upatikanaji wa elimu bora kwa watoto wa kike ndio maana akaanzisha utaratibu wa kujenga shule hizo ili kuweza kuwapa fursa wasichana kupata elimu bora.

## Shughuli za Uvuvi Ziwa Tanganyika Zarejeshwa

Waziri Ulega amezindua zoezi hilo katika Mwalo wa Katonga manispaa ya Kigoma Ujiji Mkoani Kigoma Agosti 15,2024 na kubain-



Wavuvi wakijiandaa kuanza shughui za Uvuvi baada ya shughuli za Uvuvi kurejeshwa Ziwa Tanganyika

isha kuwa kupumzishwa kwa shughuli za uvuvi kwa miezi mitatu kuanzia Mei 15 hadi Agosti 15 mwaka huu kulikuwa kunalenga kulinda rasilimali za uvuvi kwenye ziwa hilo.

Amesema uamuzi huo wa kupumzisha ziwa ni utekelezaji wa Mkataba wa Kikanda wa Nchi Wanachama wa Mamlaka ya Ziwa Tanganyika (LTA) Unaoweka Hatua za Usimamizi wa Uvuvi Endelevu katika Ziwa Tanganyika na Bonde lake.

Aidha, Waziri Ulega ametumia jukwaa hilo kuwaelekeza wavuvi kuwa kufunguliwa kwa shughuli za uvuvi kuendane na matumizi sahihi ya zana na njia halali zinazokubalika kisheria ili samaki walioachwa wazaliane na kuemdelea kupatikana kwa muda mrefu zaidi.

Akizungumza katika zoezi hilo Naibu Katibu Mkuu wizara ya mifugo na Uvuvi, Dk.Edwin Mhede alisema kuwa uvuvi imekuwa moja ya sekta kuu ya uchumi nchini ikiajiri watanzania milioni sita Sawa na asilimia 10 ya Watanzania wote.

"Takwimu za Mwaka 2023, zinaonesha 1.8% ya pato la Taifa linachangiwa na Sekta ya Uvuvi sambamba na kutoa ajira kwa wananchi Mil.6 ambao ni sawa na Asilimia 10 ya watanzania huku 95% ikiwa ni wavuvi wadogo hivyo sekta hiyo kuwa na mchango mkubwa kwa Taifa" amesema Mhede.

News Bulletin KIGOMA HABARI ZA MKOA
Web: http://www.kigoma.go.tz
Toleo Na. 006 Habari za Kila Mwezi 31 Agosti 2024

# TAHARIRI

Serikali ya Awamu ya Sita kupitia uongozi wa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu imefanikiwa kuongeza idadi ya mawakala katika vituo vya kuuzia mbolea ya ruzuku kutoka vituo vitano (5) kwa msimu wa 2022/2023 hadi kufikia 87 kwa msimu wa 2023/2024, jambo linaloendelea kusogeza na kupunguza adha ya upatikanaji wa huduma za pembejeo mkoani Kigoma.

Mabadiliko hayo hayakuja yenyewe bali yametokana na msingi mkubwa uliowekwa na serikali katika kuhakikisha Maendeleo ya Kilimo yanafikiwa, Jambo linalosimamiwa vizuri na Wizara ya Kilimo kupitia usambazaji wa kutosha wa mbolea katika Halmashauri zote za mkoa.

Katika kutekeleza mkakati wa Tanzania kuwa ni nchi ya viwanda na uchumi wa kati, Mkoa wa Kigoma umefanikiwa kutangaza mazao ya chikichi, Pamba, Kahawa, Tumbaku, Chai, Korosho, na Alizeti kuwa miongoni mwa mazao ya kimkakati.

Sambamba na hayo, serikali imeendelea kusimamia uzalishaji wa mazao ya chakula kama vile Mpunga, Maharage, Mahindi, Muhogo, viazi, na mazao mengine ya mbogamboga ili kukabiliana na uwezekano wa tatizo la uhaba wa chakula kwa wakazi wa Mkoa wa Kigoma.

Ili kuhakikisha kilimo endelevu kisichotegemea majira ya mvua, Wizara ya Kilimo kupitia Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe (Mb) amekabidhi mradi wa umwagiliaji Bonde la Luiche lenye ukubwa wa hekta 3000, ambapo utekelezaji wa mradi huo ni sehemu ya kutimiza maono ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kukuza kilimo cha umwagiliaji nchini.

Sambamba na mradi huo, Wizara ya Kilimo inaendelea na usanifu katika Wilaya ya Buhigwe, Kasulu Vijijini na Kakonko kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miradi mikubwa ya Skimu za umwagiliaji ili kuwatoa wananchi katika mfumo wa kilimo cha msimu.

Mkoa umeendelea kuimarisha mnyororo wa Thamani katika mauzo ya mazao ya kilimo ambapo kwa kushirkiana na wadau mbalimbali wa Kilimo kama Shirika la Maendeleo la Ubelgiji (Enabel) wananchi wamejengewa uwezo katika mfumo wa kilimo biashara ikiwemo uzalishaji, usindikaji na upatikanaji wa masoko kwaajili ya kuuza mazao kwa bei yenye tija kupitia vikundi vya wakulima.

Mkoa unaendelea kuwaalika wawekezaji katika Sekta ya Kilimo kutokana na uwepo wa maeneo na mazingira ya jumla yanayoruhusu kufanyika kwa uwekezaji huo kiwemo maboresho makubwa ya miundombinu ya barabara zinazouunganisha mkoa na mikoa pamoja na nchi jirani, mkoa kuunganishwa umeme wa gridi ya Taifa, ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR pamoja na kuimarika kwa masoko ya kimkakati yanayoendelea kuchechemua uchumi wa wakazi wa mkoa na maeneo jirani.

*WAHARIRI*

Gabriel Donald Ng'honoli

Andrew Ginton Mlama

*MAWASILIANO*

MKOA WA KIGOMA

Anuani: S.L.P 125

Simu: 0282802330

Simu ya kiganjani: +25576685404

Barua Pepe: ras@kigoma.go.tz / ras.kigoma@tamisemi.go.tz

News Bulletin Web: http://www.kigoma.go.tz KIGOMA HABARI ZA MKOA
Toleo Na. 006 Habari za Kila Mwezi 31 Agosti 2024

# Serikali ya Awamu ya Sita yaonesha kwa Vitendo Kuufungua Mkoa wa Kigoma




Balozi Dkt, Emanuel John Nchimbi Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapnduzi CCM

Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi amesema Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea kutekeleza kwa vitendo dhamira yake ya kuufungua Mkoa wa Kigoma sambamba na kuufanya kuwa kitovu cha Biashara kwa ukanda wa Magharibi.

Mhe. Dkt. Nchimbi ametoa kauli hiyo alipozungumza na wakazi wa wilaya ya Kasulu akiwa kwenye ziara yake mkoani hapa ambapo ameambatana na wajumbe wa Sekretariet ya CCM Taifa kwa lengo la kuhuisha chama, kusikiliza na kutatua kero za wananchi pamoja kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika uchaguzi wa Serikali za mitaa.

Amesema Rais Dkt. Samia ametoa zaidi ya Shilingi Tril. 11 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbaki ya maendeleo ikiwemo uboreshaji mkubwa wa miundombinu ya kijamii sambamba na ile wezeshi kiuchumi.

"Kuna hatua kubwa ya kimaendeleo imefikiwa hapa mkoani Kigoma katika utekelezaji wa miradi ikiwemo ujenzi wa barabara, ukarabati wa Meli, upanuzi wa uwanja wa ndege, sambamba na miradi mbalimbali ya kutolea huduma za jamii, hizi zote ni kazi nzuri zinazotekelezwa na serikali ya awamu ya sita mkoani hapa" amesisitiza Dkt. Nchimbi.

Katika hatua nyingine Dkt. Nchimbi amepokea kero mbalimbali za wananchi wilayani Kasulu na kumuelekeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI kuelekeza kiasi cha Shilingi Mil. 200 kwa ajili ya ukamilishaji wa Kituo cha Afya cha Mwami Ntale kilichopo Halmashauri ya Mji Kasulu.

Sambamba na agizo hilo, Dkt. Nchimbi amemuelekeza waziri huyo kufuatilia na kuhakikisha unapatikana ufumbuzi wa changamoto inayosababisha Kata ya Kagerankanda kukosa Diwani.

Katika hatua nyingine Balozi Dkt. Nchimbi amemuagiza Waziri wa Nishati kufuatilia na kutatua changamoto ya kukatika mara kwa mara kwa huduma ya Umeme wilayani Kasulu.

# Mchengerwa atoa miezi sita kutowepo vifo vya mama wajawazito Kigoma

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) amemuagiza Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kigoma kuweka mipango madhubuti kwa kushirikiana na wataalam wa Afya ili kutokomeza vifo vya Mama wajawazito mkoani Kigoma.

Waziri Mchengerwa ametoa maelekezo hayo alipotembelea na kukagua Maendeleo ya ujenzi wa Hospitali ya Manispaa ya Kigoma Ujiji akiwa katika ziara yake ya kikazi ya Siku Tatu mkoani hapa iliyolenga kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo sambamba na kusikiliza na kutatua kero za wananchi.

"Nakuagiza ndani ya kipindi cha Miezi Sita kuanzia leo Agosti 12, 2024 kutoendelea kutokea kwa vifo vya wanawake wajawazito kwa sababu ambazo zinaweza kuzuilika, kwani serikali imewekeza kiasi kikubwa cha Fedha kwa ajili ya kutoa huduma bora kwa na kuzuia vifo vya mama wajawazito" amesema Mchengerwa

Aidha Waziri Mchengerwa ametoa wito kwa watoa huduma za Afya nchini kuzingatia utoaji huduma bora ikiwemo kuzingatia miiko na kanuni za utumishi wao, uadilifu na kutanguliza uzalendo katika kuihudumia jamii.

"Sitosita kuchukua hatua za kinidhamu kwa mtumishi yeyote atakayebainika kupokea fedha kwa ajili ya kutoa huduma za Afya sambamba na kushindwa kutekeleza wajibu wake kuendana na miongozo ya utumishi wake" amesisitiza Waziri Mchengerwa

Katika hatua nyingine, Mhe. Waziri amemuelekeza Mkurugenzi wa Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe OR TAMISEMI kufuatilia Fedha serikali kiasi cha Shilingi Bil.2 kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo 16 katika Hospitali ya Manispaa ya Kigoma Ujiji.

Sambamba na agizo hilo Mchengerwa amemuelekeza Mkurugenzi huyo kufuatilia ili serikali iweze kutoa kiasi cha Shilingi Mil. 300 kwa ajili ya kukamilisha kituo cha Afya Kagunga kilichopo Halmashauri ya wilaya ya Kigoma na kukiwezesha kutoa huduma ili kuwaondolea wananchi adha ya kufuata huduma za matibabu nchi jirani ya Burundi

Kupitia ziara hiyo, Mhe. Mchengerwa ametoa pongezi kwa Wakala wa Barabara vijijini na Mijini (TARURA) kwa kuyaunganisha maeneo mbalimbali ya mkoa kupitia ujenzi wa madaraja ya mawe ambayo ujenzi wake hutumia gharama nafuu na kuipunguzi mzigo serikali.

Akikagua ujenzi wa barabara ya Ujiji Bangwe kwa kiwango cha Lami yenye urefu wa Km.7 inayotekelezwa chini ya mradi wa TACTICS, Mhe Mchengerwa ameonesha kutoridhishwa na mkandarasi anayetekeleza



Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI akipokea Taarifa ya Ujenzi wa Hopsitali ya Halmashauri ya Kigoma Ujiji

za mradi huo kutokana na kuwa nyuma katika utekelezaji wa mradi tofauti kwa Asilimia 18 badala ya 60 ya mkataba wake ambapo amesisitiza kuwa serikali itafuatilia ili kuwabaini wakandarasi wote wanaochelewesha miradi ili wasipewe tena kazi za miradi kama hiyo.

News Bulletin KIGOMA HABARI ZA MKOA
Web: http://www.kigoma.go.tz
Toleo Na. 006 Habari za Kila Mwezi 31 Agosti 2024

# Bado kuna Fursa nyingi za Kuwekeza Mkoani Kigoma-Rugwa

Katibu Tawala Mkoa wa Kigoma Mhe. Hassan Rugwa amesema Mkoa wa Kigoma ni miongoni mwa mikoa yenye mazingira rafiki kiuwekezaji nchini kutokana na hali yake kijiografia, kuendelea kuimarika kwa miundombinu ya uchukuzi na kutolea huduma za jamii pamoja na kupakana na nchi jirani za Burundi, Congo DR na Zambia.

Mhe. Rugwa ametoa kauli hiyo alipozungumza wakati akifungua semina ya uhamasishaji wa uwekezaji wa ndani mkoa wa Kigoma iliyolenga kujadilina kubainisha fursa zilizopo mkoani hapa, iliyoratibiwa na Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kigoma na kufanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kigoma.

Amesema serikali ya awamu ya Sita imewekeza zaidi ya Shilingi Tril.12 mkoani Kigoma kwa ajili ya kuchechemua uchumi wa Mkoa na wananchi kwa ujumla kupitia fursa zilizopo kupitia uboreshaji mkubwa wa miundombinu ya kutolea huduma za jamii, uchukuzi na usafirishaji pamoja na kuimarisha masoko ya kimkakati.

Rugwa amesema amezitaja fursa hizo kuwa zipo katika sekta ya Kilimo, Uvuvi, biashara, mifugo sambamba na uwekezaji kupitia viwanda mbalimbali.

"Nitumie nafasi hii kuwahimiza kuzitazama fursa hizo ili wafanyabiashara muweze kuwekeza katika maeneo hayo kutokana na serikali kuandaa mazingira wezeshi kwa ajili ya kufanimisha uwekezaji wenu" amesema Rugwa.

Amesema barabara zinazouunganisha mkoa na mikoa jirani zimeshakamilika kwa kiasi kikubwa huku usafiri wa anga ukiendelea kuimarika kufuatia serikali kufanya upanuzi wa uwanja wa ndege wa Kigoma kutoka Km 2 hadi kufikia Km.3.5 ili kuruhusu ndenge za kimataifa kutua mkoani Kigoma.

Upande wa Ardhi, Mhe Rugwa amesema sambamba na mkoa kuwa na maeneo mengi ya wazi yanayoruhusu kufanya uwekezaji ikiwemo ujenzi wa viwanda au kuanzisha Kilimo cha mazao ya kimkakati, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa imetenga kiasi cha hekta 140 kwa ajili ya uwekezaji katika eneo maalum la uwekezaji la mkoa (Kigoma Special Economic Zone-KiSEZ)

'Niwahimize wafanyabiashara kuwekeza katika kilimo cha zao la chikichi ili kukabiliana na uhaba wa mafuta ya kupikia ndani na nje ya mkoa sambamba na kuwekeza kwenye ardhi kama walivyofanya wawekezaji katika kiwanda cha Sukari Kasulu"amesema.

"Upande wa Afya, Serikali inajenga Hospitali ya Kanda sambamba na Tawi la Chuo Kikuu cha Muhimbili ambacho kitakuwa na wanafunzi kati ya 3000 hadi 10,000, idadi hiyo ya wanachuo ni kubwa sana hivyo itatoa fursa ya kiuchumi kwa wenye nyumba za kupangisha pamoja na wafanyabiashara ndogondogo" amesema Rugwa.

Amesema sambamba na hayo serikali iko kwenye hatua za mwisho kuunganisha mkoa na gridi ya Taifa ili kutatua changamoto ya muda mrefu ya kutotosheleza kwa umeme mkoani Kigoma.

Upande wake mshiriki wa Semina hiyo ambaye pia ni mfanyabiashara mkoani hapa Mousen Abdallah ameishauri serikali kupitia kikao hicho kukutana na wafanyabishara wa nchi jirani ya Congo DR ili waweze kujadili na kuondoa changamoto mbalimbali za kibishara.

Aidha ameiomba serikali kuandaa mafunzo ya pamoja baina ya wafanyabiashara wa Kigoma yatakayolenga kuwajengea uwezo katika kutambua majukumu ya Kituo cha uwekezaji cha Taifa jambo litakalowapa fursa ya kutambua namna bora ya kukopa na kuendesha mitaji yao kwa kuzingatia kanuni mbalimbali za kwa faida.



Baadhi ya Washiriki wa Semina ya uhamasishaji wa uwekezaji wa ndani mkoa wa Kigoma

News Bulletin KIGOMA HABARI ZA MKOA
Web: http://www.kigoma.go.tz
Toleo Na. 006 Habari za Kila Mwezi 31 Agosti 2024

# Kilio cha Wakazi wa Kata ya Mwandiga cha Mfikia Katibu Mkuu wa CCM Taifa

Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi ameendelea na ziara yake mkoani hapa ambapo akiwa njiani kwenda wilayani Kasulu amepata fursa ya kusikiliza kero kisha kuzungumza na wakazi wa Kata ya Mwandiga kisha kumuelekeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kuhakikisha unafanyika ujenzi wa Kituo cha Polisi na kusisitiza kuwa kituo hicho kikamilike Ifikapo Oktoba 2025.

Aidha amemuelekeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia kwa Naibu Waziri wa Wizara hiyo Mhe. Zainab Katimba kuhakikisha ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kata ya Mwandiga unafanyika na kukamilika ifikapo Oktoba 2025.

Sambamba na Maagizo hayo, Katibu Mkuu amesisistiza kuendelea kwa kasi kazi ya usambazaji wa Huduma ya Maji na Umeme katika Halmashauri ya Kigoma vijijini ili kurahisisha upatikanaji wa huduma hizo muhimu kwa wananchi.



Balozi Dkt, Emanuel John Nchimbi Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapnduzi CCM

# Maafisa Ugani Kilimo Wachekelea Neema ya Rais Dkt Samia



**Magari yaliyotolewa** kwa **Maafisa Kilimo kwa ajili ya Ufuatiliaji**

Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Mhe. Thobias Andengenye ameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Wizara ya Kilimo kwa kuendelea kufanya mageuzi makubwa kwenya Sekta ya Kilimo kwa lengo la kuwawezesha wakulima kufanya kilimo biashara chenye Tija.

Mhe. Andengenye ametoa kauli hiyo alipozungumza kwenye hafla ya kukabidhi vitendea kazi kwa maafisa Ugani Kilimo mkoa wa Kigoma na kusisitiza nyenzo hizo kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa na Serikali.

Amesema sekta hiyo ni muhimu kwa ustawi wa Jamii mkoani Kigoma kutokana na zaidi ya Asimilia sabini ya wakazi kutegemea shughuli za kilimo kama chanzo chao kikuu cha uchumi kwa ajili ya kuendesha maisha yao ya kila siku.

"Pamoja na Mchango mkubwa wa sekta hiyo katika mkoa wa Kigoma bado wakazi wanafanya kilimo cha kujikimu hivyo dhamira ya serikali ni kufanya mageuzi makubwa kutoka aina hiyo ya Kilimo na kuingia katika mfumo wa kilimo biashara" amesema Andengenye.

Kupitia hafla hiyo, mkuu huyo wa Mkoa amegawa magari mawili(2) yaliyotolewa na Wizara ya Kilimo kwa ajili ya kuratibu shughuli za kilimo ngazi ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na katika Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe pamoja na mavazi 179 kwa ajili ya Maafisa Ugani Kilimo ngazi ya Mkoa na Halmashauri.

Aidha Mhe. Andengenye amezikumbusha halmashauri kutekeleza maagizo ya Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe ikiwemo halmashauri ya Kigoma Ujijiku kutenga eneo ili wizara hiyo iweze kutekeleza mradi wa ujenzi wa Kituo cha kuratibu shughuli za umwagiliaji nchini.

News Bulletin KIGOMA HABARI ZA MKOA
Web: http://www.kigoma.go.tz
Toleo Na. 006 Habari za Kila Mwezi 31 Agosti 2024

# Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii Wakabidhiwa Usafiri

Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii Mkoani Kigoma wameishukuru serikali kwa kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa Sekta ya Afya ili kuweka mazingira rafiki yanayowezesha michango ya wadau hao kuigusa jamii kwa kurahisisha utoaji na upatikanaji wa Huduma.

Wakizungumza mara baada ya kukabidhiwa baiskeli ikiwa ni ufadhili kutoka Shirika lisilo la kiserikali Catholic Relief Services (CRS) kwa ajili ya kurahisisha utuatiliaji na utoaji wa huduma, baadhi ya wanufaika wa nyenzo hizo za usafiri wamesema kupatikana kwa vitendea kazi hivyo kutasaidia kuifikia namba kubwa ya wateja wao na kwa wakati sahihi.



Honorina Sunzu ambaye ni muhudumu wa Afya ngazi ya Jamii kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma anasema awali walikuwa wakitumia muda mrefu kuwafikia walengwa jambo lililosababisha baadhi yao kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

"Nyenzo hizi zimeamsha ari katika utendaji kazi wetu, hivyo tunaishikuru serikali kwa kushirikiana na wadau wa Afya kwa kuiona changamoto hii iliyokuwa ikitukabili kisha kuamua kuitatua" amesema.

Mkuu wa Shirika lisilo la kiserikali la Catholic Relief Services Tanzania (CRS) Taylor Lanton amesema Shirika hilo limetoa Baiskeli 250 ambapo kati ya hizo 200 ni kwa ajili ya wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii pamoja na walimu wa Vijiji kwa ajili ya vikundi vya kuweka na kukopa vijijini ili kuwaaezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Amesema mojawapo ya majukumu ya msingi ya Shirika hilo ni kutekeleza mradi unaolenga kuboresha hali za afya na lishe kwa vijana walio katika rika balehe waliopo shuleni na kwenye Jamii sambamba na wanawake vijana wenye umri kati ya miaka 10 hadi 24 mkoani Kigoma.

"Tunaendelea kuangalia zaidi katika kuiongezea nguvu serikali katika kuboresha Afya ya Jamii, uwepo wa lishe bora sambamba na kuboresha maisha ya mtu mmoja mmoja kupitia maeneo hayo, aidha nimefurahishwa na namna mnavyoutekeleza mradi pamoja na ushirikianomkubwa mnaotupa kama uongozi wa mkoa wa Kigoma nasi tunaendelea kuahidi kufanya kazi nanyi" amesema Bi. Lyton.

Akizungumza kabla ya kukabidhi vitendea kazi hivyo Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Mhe. Thobias Andengenye amesema Serikali ya awamu ya Sita kupitia wizara ya Afya itaendelea kushirikiana na wadau wa Maendeleo kupitia sekta hiyo ili kukabialiana na changamoto zinazowakabili wananchi hususani katika upatikanaji wa huduma bora za Afya.

Amewataka wanufaika wa vitendea kazi hivyo kwenda kuvitumia kuendana na miongozo waliyopewa ili viweze kuleta ufanisi katika Mapinduzi ya Sekta hiyo muhimu sambamba na kupunguza idadi ya vifo vya wanawake wajawazito na watoto katika maeneo ya vijijini.

"Nichukue nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza wahudumu wote wa Afya ngazi ya Jamii mkoa wa Kigoma kwa kazi nzuri mnazozifanya ambazo zimekuwa na mchango mkubwa katika kuboresha Afya, lishe na Ustawi wa watu wa Kigoma kwa jumla"amesisitiza Andengenye.

Jumla ya baiskeli 72 zimegawiwa katika halmashauri ya Kigoma, 84 Wilaya ya Uvinza na nyingine 94 zikitolewa kwa wanufaika katika halmashauri ya wilaya ya Kibondo.

News Bulletin KIGOMA HABARI ZA MKOA
Web: http://www.kigoma.go.tz
Toleo Na. 006 Habari za Kila Mwezi 31 Agosti 2024

# Mashirika yasiyo ya Kiserikali yachangia Maendeleo Mkoani Kigoma

Katibu Tawala Mkoa wa Kigoma Mhe. Hassan Rugwa amesema uwepo wa Mashirika yasiyo ya kiserikali mkoani Kigoma umechangia kuisaidia serikali kwa kiasi kikubwa katika kutatua changamoto za wananchi kupitia utekelezaji wa afua mbalimbali kwa lengo la kusukuma mbele gurudumu la maendeleo.



Hassan Abbas Rugwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma

Mhe. Rugwa ametoa kauli hiyo alipofungua Mkutano wa Mashirika yasiyo ya kiserikali mkoa wa Kigoma uliolenga kupitia taarifa za utendaji kazi wa Mashirika hayo kwa kipindi cha Januari hadi Desemba 2023 na kusisitiza kuwa wadau hao wamekuwa mchango mkubwa kupitia afua mbalimbali wanazotekeleza ikiwemo kwenye sekta ya toaji wa huduma za jamii, Maendeleo ya Jamii, utawala bora, sambamba na utunzaji wa Mazingira.

Kupitia hotuba yake, kiongozi huyo amezitaja changamoto mbalimbali zinazoyahusu mashirika hayo kuwa ni pamoja na kutegemea zaidi wafadhili katika utekelezaji wa majukumu yao hivyo ufadhili unapokoma au kulegalega husababisha ufanisi wa mashirika hayo kuwa mdogo au kushindwa kabisa kujiendesha na kusababisha baadhi ya mipango kutokamilika.

"Hali hii huchangia kwa kiasi kikubwa mashirika mengi kutekeleza majukumu kwa kuzingatia matakwa ya wafadhili badala ya kuzingatia mahitaji halisi ya wananchi katika mazingira waliyopo"amesema Rugwa Ameitaja changamoto nyingine kuwa ni mashirika mengi kutekeleza majukumu yao katika maeneo ya mijini badala ya kujielekeza vijijini ambapo pia kuna mahitaji makubwa ya kijamii.

"Niwasisitize kuzingatia na kujielekeza maeneno yote ya mijini na vijijini mnapoweka mipango ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili wanakigoma wote waweze kunufaika na utendaji kazi wenu" amesema Rugwa.

Rugwa ameyataka mashirika hayo kutoa taarifa za utekelezaji wa kazi zao kwa wananchi katika maeneo wanayotoa huduma ili wakazi waweze kufahamu maendeleo na matokeo ya kazi hizo wanazozifanya.

Aidha kupitia hotuba yake, Katibu Tawala ameyataka Mashirika hayo kujenga utamaduni wa kufanya utafiti utakaoshirikisha wananchi ili waweze kutoa maoni kuhusu mahitaji yao ili huduma zinazotolewa na mashirika hayo ziweze kuwagusa moja kwa moja. Utakuta kuna maeneo yanamashirika zaidi ya moja na kazi wanazofanya zinafanana, hivyo niwatake mkafanye utafiti na kutawanya huduma zenu katika maeneo yote ya mkoa badala ya kujikita mijini au katika halmashauri chache huku maeneo mengine yakikosa huduma.Aidha katibu tawala huyo ameahidi kuendelea kutoa ushirikiano kwa mashirika hayo ili yaweze kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi katika kuhakikisha wananchi wa mkoa wa Kigoma wanapata huduma muhimu




Washiri mbalimba wa Mkutano wa Mashirika yasiyo ya kiserikali Mkoani wa Kigoma

# Mfumo wa M-MAMA wakabidhiwa rasmi kwa Serikali aya Mkoa wa Kigoma

Wakurugenzi watendaji wa Halmashauri za Wilaya za Wilaya Mkoani hapa wametakiwa kuongeza kasi ya uchangiaji fedha kwenye mfumo wa M-Mama sambamba na kuwalipa Madereva Jamii wanaoendesha magari yanayotoa huduma hiyo ili kuwezesha zoezi la kuwafikisha wajawazito na watoto katika vituo vya kutolea huduma za Afya kwa wakati.

Akizungumza kwenye kikao cha wadau cha kukabidhi Mfumo wa M-Mama kwa Serikali ya mkoa wa Kigoma, kwaniaba ya Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa wilaya ya Kigoma Salum Kalli amesema iwapo Halmashauri zitaupokea mfumo huo na kuzingatia miongozo ya uendeshaji




Mkuu wa Wilaya ya Kigoma Salum Kalli akionesha nyaraka ya Makabidhiano ya Mradi wa M-MAMA

wake itasaidia kuendelea kupunguza vifo vya wanawake na watoto ili kudumisha uzazi salama.

Mhe. Kalli amesema watendaji hao kwa kushirikiana na wasimamizi wa mfumo wanapaswa kuimarisha uwajibikaji ili kuufanya mfumo huo kuwa endelevu na kutimza dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuhakikisha changamto ya vifo vya wajawazito, wanawake wanaojifungua pamoja na watoto inamalizika mkoani Kigoma.

Kupitia kikao hicho Mhe. Kalli amewahimiza wakazi mkoani hapa kuzingatia ulaji mlo kamili ili kulinda Afya zao dhidi ya maradhi yanayoweza kuzuilika kupitia ulaji wa chakula bora.

Katika hatua nyingine Mkuu huyo wa Wilaya amewataka wakazi mkoani hapa kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya maradhi mbalimbali ikiwemo kuzingatia kaninu za Afya pamoja na namna bora ya kujikinga na magonjwa ya mlipuko.

Upande wake mratibu wa Mfumo ngazi ya Mkoa Bernadetha Peter amesema, jumla ya wateja 2,598 wamefanikiwa kusafirishwa ili kuvifikia vituo vya kutolea huduma ya Afya tangu kuanzishwa kwa mfumo huo mkoani Kigoma Aprili 20,2024 huku idadi ya wanawake ikiwa 2,220 na watoto 368.

Amesema mara baada ya mfumo kukabidhiwa serikalini, wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanapaswa kuhakikisha Idara ya Fedha na Afya katika halmashauri zao zinasimamia uendeshaji wa mfumo kwa kuzingatia maelekezo yanayotolewa na seikali ili kufikia malengo yaliyowekwa

Ameeleza kuwa, Mfadhili Mkuu wa Mradi Kampuni ya Vodafone kwa kushirikiana na wadau wanaotekeleza uendeshaji wa mfumo huo Shirika la Pathfinder International pamoja na Touch Health wanakabidhi rasmi mfumo huo katika mamlaka ya Mkoa hivyo Halmashauri zitapaswa kuendeleza majukumu ambayo wadau hao walikuwa wakiyatekeleza.

Ameyataja mambo ya kuzingatia ili halmashauri ziweze kufanikiwa katika utekelezaji mpango huo kuwa ni pamoja na wafawidhi wa vituo kusimamia rufaa zote za mama na mtoto ili ziwe kwenye mfumo wa M-Mama, kuidhinisha malipo sahihi na kwa wakati kwa madereva Jamii pamoja na waganga wakuu na kamati za Afya wilaya kusimamia na kutoa taarifa kwa wakati.

"Nitoe rai kwa Uongozi wa Halmashauri kufanya malipo ya madereva kwa wakati sambamba na kuhakikisha gari za kusafirisha wagonjwa zinakuwa na mafuta ya kutosha ili ziweze kutumika muda wowote inapohitajika kufanyika hivyo" amesema Mratibu wa mfumo huo Bernadetha Peter.

Aidha ameyataja mafanikio ya mpango huo tangu ulipoanzishwa mkoani Kigoma kuwa ni pamoja na vituo vyote 291 kutumia Namba 115 wakati wa dharura ya mama na mtoto, uelewa wa jamii na wadau wote kuhusu umuhimu wa mfumo huona kuhakikisha unaimarika sambamba na kuendelea kufanyika kwa mawasiliano ya haraka miongoni mwa watumiaji wa mfumo.

# Mchengerwa aibana TARURA Barabara Wanazojenga Mkoani Kigoma

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) amememuelekeza Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini nchini TARURA Mkoa wa Kigoma kuweka taa katika barabara zote zinazojengwa na wakala huyo mkoani Kigoma ili kudumisha usalama nyakati za usiku sambamba na kupendezesha miji katika maeneo zilipo barabara hizo.

Mhe. Waziri Mchengerwa ametoa maelekezo hayo alipokagua mradi wa ujenzi wa barabara iliyojengwa kwa kiwango cha lami Km. 1.1 kutoka Ujenzi hadi GTZ na Kiganamo hadi Bogwe katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu, akiwa katika ziara yake ya kikazi mkoani hapa.

Amesema Mhe.Rais Dkt. Samia amelenga kuendelea kuimarisha miundombinu ya barabara mkoani Kigoma ili kuvutia wawekezaji na wafanyabiashara kupitia sekta hiyo muhimu ya uchukuzi sambamba na kuboresha mazingira ya miji katika mkoa huo na Tanzania kwa ujumla.

Ujenzi wa barabara hizo kwa kiwango cha lami nyepesi umegharimu kiasi cha Shilingi Mil. 950, fedha kutoka serikali kuu na kukamilika kwake kumetajwa kuwaondolea adha ya ubovu wa barabara wakazi wa mji huo na kuzifanya zipitike kwa wepesi nyakati za masika na kiangazi.

Awali akiwa waziri huyo ametembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa Kituo cha Afya Mwami Ntale kilichopo katika Halmashauri hiyo na kumuagiza Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo kumbadilishia Kituo cha Kazi Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji Kasulu Dkt.Peter Janga kutokana na kutoridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho.

"Haiwezekani kituo kifunguliwe na kukosa Samani kwa kipindi cha zaidi ya Mwaka, huku kikiwa hakina Umeme na majengo kutotosheleza, hii haikubaliki na nnakuagiza Katibu Mkuu kumbadilishi kituo cha kazi sambamba na kuitaka TAKUKURU kufika hapa na kuanza uchunguzi wa ujenzi wa mradi huu"amesema mchengerwa

Katika hatua nyingine Waziri Mchengerwa ameiagiza TAKUKURU kufanya uchunguzi katika Shule ya Sekondari Nyumbigwa Mpya kupitia Program ya P4R kwa kiasi cha Shilingi Bil. 1 na fedha hizo kumalizika huku baadhi ya miundombinu ya Shule ujenzi wake kutokuwa umekamilika.

Kupitia ziara hiyo, Waziri Mchengerwa amesikiliza na kupokea kero za wananchi katika kata ya Kagerankanda ikiwemo uwepo wa changamoto ya uwepo wa migogoro ya ardhi, kata hiyo kutokuwa na diwani tangu mwaka 2021 sambamba na ombi la kupandishwa hadhi kwa shule ya sekondari kimenyi hadi kufikia kidato cha Sita.

Akitoalea ufafanuzi jero hizo za wananchi, Waziri huyo ameahidi kupeleka wataalam kutoka Wizara hiyo wanaoshughulikia masuala ya



Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) Waziri wa Nchi Ofifi ya Rais TAMISEMI akisisitiza jambo mbele ya Viongozi wa Mkoa wa Kigoma

Elimu ili kuona kama Shule hiyo ya Sekondari ya Kimenyi inakidhi vigezo vya kupandishwa hadhi hadi kutoa Elimu ya Kidato cha Sita.

Sambamba na hilo, waziri Mchengerwa ameahidi kukutana na Diwani wa Kata hiyo aliyesimamishwa kwa changamoto za masuala ya uraia ili kufahamu kiwango cha utatuzi wa changamoto zake ili aweze kurudi kuwatumikia wananchi.

Kuhusu suala la migogoro ya ardhi, Mchengerwa ameahidi kurudi katia kata hiyo ndani ya kipindi cha Siku 30 akiwa na Waziri mwenye dhamana ya ardhi ili kutatua na kuzitolea maamuzi changamoto ambazo wananchi hao wanankutana nazo kupitia sekta hiyo.